# I. Kuzimwa kwa mtandao mnamo 2022: mtazamo wa kimataifa

# Muhtasari wa data ya 2022

## Idadi ya kufungwa mtandao iliyosajiliwa*

| Mwaka | Jumla ya idadi ya kuzimwa mtandao | Jumla ya idadi ya kufungwa mtandao, India ikiwachwa kando |
|---|---|---|
| 2016 | 75 | 45 |
| 2017 | 106 | 37 |
| 2018 | 196 | 62 |
| 2019 | 213 | 92 |
| 2020 | 159 | 50 |
| 2021 | 184 | 77 |
| 2022 | 187 | 103 |

*Nambari hizi zinaonyesha data ya hivi punde inayopatikana tangu kuchapishwa kwa ripoti hii na inajumuisha masahihisho ya jumla yaliyochapishwa hapo awali kwa miaka iliyopita.

## Idadi ya nchi zilizokumbwa na kuzimwa kwa mtandao

| 2016 | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 25 | 19 | 26 | 33 | 29 | 34 | 35 |



**India:** 84
**Ukreni:** 22**
**Irani:** 18
**Myanmar:** 7
**Bangladeshi:** 6ii
**Jordan:** 4i
**Libya:** 4
**Sudani:** 4
**Turkmenistani:** 4

**Afghanistan:** 2 **Burkina Faso:** 2 **Cuba:** 2 **Kazakhstan:** 2 **Urusi:** 2 **Sierra Leone:** 2 **Tajikistan:** 2 **Uzbekistani:** 2

**Algeria:** 1 **Armenia:** 1 **Azerbaijani:** 1 **Brazil:** 1 **Uchina:** 1 **Ethiopia:** 1 **Iraki:** 1 **Nigeria:** 1 **Omani:** 1 **Pakistani:** 1 **Somaliland:** 1 **Sri Lanka:** 1 **Syria:** 1 **Tunisia:** 1 **Uturuki:** 1 **Uganda:** 1 **Yemen:** 1** **Zimbabwe:** 1

**Kuzimwa kwa mtandao kulishurutishwa na msukumo kutoka nje wakati wa vita vya kijeshi huko Ukreni na Yemen.

# Visababishi vya kuzimwa mtandao mwaka wa 2022

## Maandamano

Maandamano katika nchi **16** yalisababisha kuzimwa mtandao **62**

## Mitihani

Mtandao ulizimwa mara **8** katika nchi **6** ili kusitisha "udanganyifu kwenye mitihani"

## Migogoro ya kivita

Mtandao ulizimwa mara **33** wakati wa migogoro ya kivita

## Uchaguzi

Mtandao ulizimwa mara **5** katika nchi **5** kwa ajili ya uchaguzi

# Mielekeo Ya Kuzimwa Kwa Mitandao mwaka wa 2022

## 1. Ukiukaji mkubwa wa haki za kibinadamu*** na ziada ya vurugu zinazosababishwa na kufungwa mtandao

→ Mtandao ulizimwa mara **48** katika nchi **14** zilisajiliwa kwa sababu ya ukiukaji mkubwa wa haki za kibinadamu

Bangladeshi, Ethiopia, Irani, Jodan, Kazakhstani, Myanmar, Urusi, Sierra Leone, Somaliland, Sudani, Tajikistani, Uzbekistani, pamoja na sehemu mbili ambamo vita bado vinaendelea -Ukreni and Yemen.

*** Ukiukaji wa haki za binadamu ni pamoja na kesi ambapo kuna ushahidi wa vurugu, ikiwa ni pamoja na mauaji, mateso, ubakaji, au uhalifu wa kivita unaoonekana kufanywa na serikali, wanajeshi, na polisi au vikosi vya usalama.

## 2. Nchi zinazorudiarudia makosa na zinazokuwa na mida mirefu ya kuzimwa mtandao

→ **Siku 787 na zaidi**

Kufikia mwisho wa mwaka wa 2022, watu huko Tigray, Ethiopia walikuwa wamevumilia miaka **2** na zaidi ya kukatika kwa mawasiliano kamili, na wengi bado hawajaunganishwa.

→ **33** kati ya nchi **35** zilizozima mtandao ni wakosaji wa kurudia tangu 2016

→ **Siku 500 na zaidi**

Watu katika mikoa mingi kote Myanmar walikuwa wamekaa gizani kwa siku 500 na zaidi kufikia Machi 2022.

→ Mara **16** ulimwenguni kote kuzimwa kwa mtandao kuliendelea kutoka 2021 hadi 2022 na hali **16** sasa zinaendelea kutoka 2022 hadi 2023, ikilinganishwa na **8** kati ya 2020 na 2021

## 3. Kuzimwa mtandao na athari zake na maafa yasiyokadirika

→ Nchi **23** walizima mtandao mara **28** mwaka wa 2022 kwa sababu za huduma husika.

Afghanistani, Algeria, Armenia, Azerbaijani, Bangladeshi, Brazili, Burkina Faso, Uchina, India, Irani, Jodan, Kazakhstani, Nigeria, Oman, Urusi, Sri Lanka, Tunisia, Turkmenistani, Uganda, Ukreni, (iliyowekwa kwa nguvu na Jesho la Urusi), Uzbekistan, and Zimbabwe.

→ Mbinu tofauti tofauti za kuzima mtandao+, udhibiti + ufuatiliaji:

**Uajemi:** Vizuizi katika mi<tandao kote nchini + hadhari ya mtindo wa kutoruhusu watu kutoka nje katika maeneo maarufu ya kanda

**Myanmar:** Kutatiza mitandao ya simu za rununu, ukwamishaji wa VPN, ujumbe wa kitaalamu ulodhibitiwa+ kulazimisha watu kwenye mitandao ya ISP inayofuatiliwa sana, inayoendeshwa na jeshi.

**Ukreni:** Mashambulizi ya mtandaoni yanaathiri Watoa Huduma za Intaneti wa Ukreni + majaribio ya kulazimisha maeneo yaliyokaliwa kwenye mitandao ya Urusi iliyodhibitiwa sana na iliyochunguzwa.

## Africa
## Mtazamo wa Eneo Husika mwaka wa 2022

**19** Kuzimwa mara
**12** Nchi
2021

**9** Kuzimwa mara
**7** Nchi
2022

# Ethiopia: 1

**Kufikia mwisho wa 2022, kuzimwa mtandao huko Tigray imefikia siku 787**

# Uganda: 1

**Kufikia mwisho wa mwaka wa 2022, Kufungwa kwa Facebook kumefikia siku 719**

**Burkina Faso:** 2 **Sierra Leone:** 2 **Nigeria:** 1 **Somaliland:** 1 **Zimbabwe:** 1

**Asilimia 44.5% ya kuzimwa kwa mtandao kulisababishwa na vurugu za kisiasa.**

Sierra Leone: 2 Somaliland: 1 Zimbabwe: 1

**Asilimia 33.3% ya kuzimwa kwa mtandao ililenga mitandao mengine ya kijamii.**

Burkina Faso: 1 Nigeria: 1 Uganda: 1

Ingawa 2022 iliweka rekodi ya chini kwa idadi ya kila mwaka ya kuzimwa mtandao katika eneo hili tangu tuanze kufuatilia mnamo 2016, Afrika bado inashikilia rekodi ya mtandao kuzimwa kwa muda mrefu zaidi ulimwenguni, katika eneo la Tigray, Ethiopia. Angalau vizuizi vinne kati ya tisa vya eneo hilo vilifanyika pamoja na ukiukaji wa haki za kibinadamu ulioripotiwa, katika muktadha wa ukandamizaji mkali dhidi ya maandamano na migogoro inayoendelea. Kihistoria uchaguzi umekuwa kichocheo kikubwa cha kuzimwa kote barani Afrika, lakini kulikuwa na chaguzi chache katika eneo hili mwaka wa 2022, na tulinakili tukio moja linaloendelea la kufungwa kwa jukwaa inayohusiana na uchaguzi nchini Uganda ambayo imekuwa tangu 2021.[1] Kwa kuwa kutakuwa na chaguzi nyingi zaidi mnamo 2023, muungano wa Access Now na #KeepItOn utaendelea kufuatilia kwa karibu hali hiyo.[2]

## Kuzima Mtandao Wakati wa Maandamano na Machafuko

Mamlaka nchini Burkina Faso, Sierra Leone, Somaliland, na Zimbabwe zote zilijibu maandamano na matukio makubwa ya kisiasa kwa kuzima mtandao.

Baada ya kujiunga na orodha ya aibu ya nchi zinazozima mtandao mnamo Novemba 2021, serikali ya Burkina Faso ilianza mwaka mpya kwa kujibu maandamano dhidi ya serikali yaliyotokea Januari 10 kwa kuzima mtandao wa simu za rununu nchini kote, bila kutoa maelezo yoyote kwa hatua zake

1 Monitor (2022). *Facebook to remain shut as govt talks with tech giant stall*. Retrieved February 22, 2023, from https://www.monitor.co.ug/uganda/news/national/facebook-to-remain-shut-as-govt-talks-with-tech-giant-stall-3912172/.

2 Access Now (2022). *2023 elections and internet shutdowns watch*. Retrieved February 17, 2023, from https://www.accessnow.org/2023-elections-and-internet-shutdowns-watch/.

hizo.[3] Ingawa mamlaka ilirejesha mawasiliano hayo siku iliyofuata, serikali iliendelea kuzuia Facebook, ikitaja "usalama wa taifa" kama sababu ya kuhalalisha hatua hiyo.[4] Wiki chache baadaye Januari 23, kufuatia ripoti za jaribio la mapinduzi, serikali kwa mara nyingine tena ilikata mawasiliano ya simu nchini kote,[5] na kurejesha mawasiliano siku mbili baadaye.[6]

Wakati maandamano dhidi ya serikali yalipoongezeka nchini Sierra Leone kutokana na kupanda kwa gharama ya maisha, mamlaka ilizima mtandao ili kuzima maandamano.[7] Mara ya mwisho kwa serikali ya Sierra Leone kuzima mtandao ilikuwa mwaka 2018, wakati wa uchaguzi.[8]

Vile vile, mamlaka katika Somaliland, nchi iliyojitangaza yenyewe ndani ya mipaka inayotambulika kimataifa ya Somalia, ilifunga ufikiaji wa mtandao katika hali ya kupinga maandamano ambayo yalizuka Agosti 2022 kufuatia kuahirishwa kwa uchaguzi wa rais.[9] Ufungaji wa mtandao huo, ambao uliathiri eneo la Woqooyi Galbeed pamoja na maeneo ya Kusini na Kati ya Somalia, ulidumu takriban masaa 10.[10] Mnamo 2017, mamlaka ya Somaliland ilifunga ufikiaji wa mitandao ya kijamii wakati wa uchaguzi.[11]

Hatimaye, serikali ya Zimbabwe ilivuruga huduma ya mtandao mara kwa mara katika jaribio la kuingilia mkutano wa "Jumapili ya Manjano" uliofanyika na chama cha upinzani cha Citizens' Coalition for Change. Wafuasi walipokusanyika kwa mkutano huo, watu walianza kuripoti ugumu wa kufikia mitandao ya kijamii[12] Zimbabwe hapo awali iliweka vikwazo vya mtandao ili kukomesha maandamano.[13]

## Vikwazo wakati wa uchaguzi

Uchaguzi, ambao mara nyingi huhusishwa na maandamano na machafuko, kwa muda mrefu umekuwa kichocheo thabiti cha kuzima mtandao barani Afrika. Kama tulivyoona, idadi ya chini ya rekodi ya kufungwa mtandao kwa ajili ya uchaguzi mwaka wa 2022 (tukio moja nchini Uganda linaloendelea kutoka 2021) kuna uwezekano kulitokana na idadi ndogo ya chaguzi zilizofanyika. Inawezekana pia kwamba utetezi wa mashirika ya kiraia ulichangia katika kuzuia mamlaka kuingiliwa.

Gambia ilikuwa kwenye orodha yetu ya ufuatiliaji wa uchaguzi,[14] na Aprili 2022, nchi hiyo iliendelea na ufikiaji wa mtandao katika muda wote wa uchaguzi wake wa wabunge, licha ya historia ya kuweka vikwazo vinavyohusiana na uchaguzi kuanzia mwaka wa 2016.[15]

Wakati huohuo, Kenya iliweka na kudumisha ahadi yake ya #KeepItOn wakati wa uchaguzi mkuu wa Agosti 2022, ikijitokeza kama kiongozi miongoni mwa

3 Desobeissance Civile. Facebook Post. January 10, 2022. Retrieved February 17, 2023, from https://www.facebook.com/Desobeissancecivileburkina/posts/4817989371573475/.

4 Anadolu Agency (2022). *Burkina Faso restricts Facebook after internet outages*. Retrieved February 17, 2023, from https://www.aa.com.tr/en/africa/burkina-faso-restricts-facebook-after-internet-outages/2480343/.

5 Faso7 (2022). Burkina Faso: *La connexion Internet mobile à nouveau coupée*. Retrieved February 17, 2023, from https://faso7.com/2022/01/23/burkina-faso-la-connexion-internet-mobile-a-nouveau-coupee/.

6 Access Now (2022). *Burkina Faso must immediately end its internet shutdown, not extend it*. Retrieved February 17, 2023, from https://www.accessnow.org/burkina-faso-internet-shutdown/.

7 Access Now (2022). *#KeepItOn in Sierra Leone: the government must stop wielding internet shutdowns for political control*. Retrieved February 17, 2023, from https://www.accessnow.org/keepiton-in-sierra-leone/.

8 African Freedom of Expression Exchange (2018). *Sierra Leone Joins Global Trend: Shuts Down Internet and Mobile Services during Elections*. Retrieved February 17, 2023, from https://www.africafex.org/digital-rights/sierra-leone-joins-global-trend-shuts-down-internet-and-mobile-services-during-elections__trashed/.

9 Access Now (2022). *#KeepItOn in Somaliland: authorities cannot quash public protest and access to information*. Retrieved February 22, 2023, from https://www.accessnow.org/keepiton-in-somaliland/.

10 *Ibid*.

11 Africa News (2017). *Somaliland to shut down social networks during election period*. Retrieved February 17, 2023, from https://www.africanews.com/2017/11/11/somaliland-to-shut-down-social-networks-during-election-period/.

12 Zimbabwe Independent (2022). *Cyberspace the new Zim political battlefield*. Retrieved February 17, 2023, from https://www.newsday.co.zw/theindependent/amp/slider/article/4091/cyberspace-the-new-zim-political-battlefield/.

13 Al Jazeera (2019). *Zimbabwe imposes internet shutdown amid crackdown on protests*. Retrieved February 17, 2023, from https://www.aljazeera.com/news/2019/1/18/zimbabwe-imposes-internet-shutdown-amid-crackdown-on-protests/.

14 Access Now (2022). *#KeepItOn: 2022 elections and internet shutdowns watch*. Retrieved February 17, 2023, from https://www.accessnow.org/elections-internet-shutdowns-watch-2022/.

15 Africa News (2016). *Gambia's Jammeh slams request to stabilize internet on election day*. Retrieved February 22, 2023, from https://www.africanews.com/2016/12/01/gambia-s-jammeh-slams-request-to-stabilize-internet-on-election-day/.

majirani zake katika Afrika Mashariki. Hiyo ni pamoja na Uganda, ambayo ilikuwa imefunga Facebook kabla ya uchaguzi mkuu wa Januari 2021 na hadi sasa haijaondoa kizuizi hicho.[16]

Wakati huohuo, Kenya iliweka na kudumisha ahadi yake ya #KeepItOn wakati wa uchaguzi mkuu wa Agosti 2022, ikijitokeza na kutimiza ahadi yake ya kutozima mtandao na kwa kufanya hivyo ikajithibitisha kama kiongozi bora wa eneo hili.[17]

Kabla ya uchaguzi wa Kenya, Waziri wa Mambo ya Ndani wa wakati huo, Fred Matiang'i, alidokeza kuwa serikali haikuwa na nia ya kuzima mtandao.[18] Hata hivyo, aliweka wazi kuwa serikali ilinuia kuchukua kwa uzito uenezaji wa habari potofu na matamshi ya chuki.[19] Baada ya utafiti wa shirika la kutetea haki za binadamu la Global Witness kufichua kwamba Facebook ya Meta iliidhinisha matangazo yenye matamshi ya chuki,[20] Tume ya Kitaifa ya Uwiano na Utangamano (NCIC) ilitishia kuifungia Meta lau isingechuka hatua za kuzuia kuenea kwa maudhui ya chuki. Shirika hilo liliipa Meta siku saba kutimiza matakwa yake.[21] Mashirika kadhaa ya kiraia na baadhi ya maafisa wa serikali walilaani tishio hili kwa kujali uhuru wa kujieleza unaozunguka uchaguzi. Hatimaye serikali ilithibitisha kuwa mtandao au mitandao ya kijamii haitazuiwa. Hatimaye serikali ilithibitisha kuwa mtandao au mitandao ya kijamii haitazuiwa.[22]

Kwa kuwa kusimamishwa kwa uchaguzi kunaasalia kuwa tishio, muungano wa Access Now na #KeepItOn utafuatilia uchaguzi katika nchi 11 barani Afrika mnamo 2023, ambazo zote ziliweka marufuku hapo awali. [23] **Hii ni fursa muhimu kwa demokrasia barani Afrika kutayarisha mkondo mpya, kwa kujitolea kwa dhati ku#KeepItOn katika vipindi vyao vyote vya uchaguzi.**

## Vizuizi vya jukwaa endelevu

Mnamo 2021, serikali za Nigeria[24] na Uganda[25] kila moja ilichukua hatua kwa kulipiza kisasi dhidi ya majukwaa ya mitandao ya kijamii ambayo yaliondoa machapisho ya viongozi wa serikali au wafuasi wao. Baada ya majukwaa kuondoa machapisho haya kwa sababu hayakutimiza masharti ya huduma, mamlaka za serikali zilizuia ufikiaji wa majukwaa haya kabisa.

Serikali ya Nigeria ilizuia ufikiaji wa Twitter kwa muda wa miezi saba kamili, na hivyo kuzua malalamiko makubwa ya umma.[26] Mamlaka iliondoa tu kizuizi hicho mnamo Januari 2022 kufuatia mazungumzo ya kina na kampuni.[27] Mashirika ya kiraia yalishtaki juu ya uhalali wa marufuku hii ya Twitter, na mwaka wa 2022, yalipata ushindi muhimu huku Mahakama ya Jumuiya ya Haki ya Jumuiya ya Kiuchumi ya Nchi za Afrika Magharibi (ECOWAS Court) ikitangaza uzuiaji huo kuwa kinyume

16 The New York Times (2021). *Uganda Blocks Facebook Ahead of Contentious Election*. Retrieved February 17, 2023, from https://www.nytimes.com/2021/01/13/world/africa/uganda-facebook-ban-elections.html/.

17 Access Now (2022). *Eyes on Kenya: government must uphold commitment to connectivity during elections*. Retrieved February 17, 2023, from https://www.accessnow.org/kenya-government-internet-connectivity-elections/; Access Now (2022). *Warning: blocking online platforms in Kenya will spread election disinformation*. Retrieved February 17, 2023, from https://www.accessnow.org/kenya-online-platforms-social-media-blocking-internet-shutdown-election/.

18 The Star (2022). *We won't shut down internet during elections - Matiang'i*. Retrieved February 17, 2023, from https://www.the-star.co.ke/news/2022-06-09-we-wont-shut-down-internet-during-elections-matiangi/.

19 The People Daily (2021). *Matiang'i: State won't switch off Internet but we're watching you*. Retrieved February 17, 2023, from https://www.pd.co.ke/news/matiangi-state-wont-switch-off-internet-but-were-watching-you-83867/.

20 Global Witness (2022). *Facebook approves ads calling for ethnic violence in the lead up to a tense Kenyan election*. Retrieved February 22, 2023, from https://www.globalwitness.org/en/press-releases/facebook-approves-ads-calling-ethnic-violence-lead-tense-kenyan-election/.

21 The East African (2022). *Kenya threatens ban on Facebook over hate speech*. Retrieved February 17, 2023, from https://www.theeastafrican.co.ke/tea/news/east-africa/kenya-threatens-ban-on-facebook-over-hate-speech-3896380/.

22 Joe Mucheru EGH (@mucheru). Twitter Post. 1:48 AM. July 30, 2022. Retrieved February 22, 2023, from https://twitter.com/mucheru/status/1553271302005334016/.

23 *See supra* note 2.

24 Access Now (2022). *Blocking access to Twitter in Nigeria is a flagrant violation of fundamental rights*. Retrieved February 22, 2023, from https://www.accessnow.org/nigeria-blocks-twitter-keepiton/.

25 The New York Times (2021). *Uganda Blocks Facebook Ahead of Contentious Election*. Retrieved February 17, 2023, from https://www.nytimes.com/2021/01/13/world/africa/uganda-facebook-ban-elections.html/.

26 The New York Times (2022). *Nigeria Lifts 7-Month Ban on Twitter*. Retrieved February 22, 2023, from https://www.nytimes.com/2022/01/13/world/africa/nigeria-lifts-twitter-ban.html/.

27 Access Now (2022). *Blocking access to Twitter in Nigeria is a flagrant violation of fundamental rights*. Retrieved February 17, 2023, from https://www.accessnow.org/nigeria-blocks-twitter-keepiton/.

cha sheria.[28]

Serikali ya Uganda, wakati huo huo, imeendelea kuzuia Facebook kwa zaidi ya miaka miwili, na kufikia Februari 2023, Waganda wanaweza tu kuipata kwa kutumia VPN.[29]

## // Ethiopia

Eneo la Tigray nchini Ethiopia limefungwa kwa huduma za mawasiliano tangu kuanza kwa vita vya wenyewe kwa wenyewe mnamo Novemba 4, 2020.[30] Makubaliano ya amani kati ya serikali ya shirikisho ya Ethiopia na chama cha Tigray People's Liberation Front (TPLF) - ambayo yanajumuisha ahadi za serikali kurejesha ufikiaji wa huduma muhimu kote kanda - ilianza kusikilizwa mnamo Novemba 2022.[31] Lakini tumeanza kuona muunganisho mdogo tu tangu Desemba 2022, wakati Ethio Telecom ilipoanza ukarabati wa miundombinu. Kufikia Februari 2023 watu wengi katika eneo hilo walisalia bila muunganisho, na wale ambao wamepata ufikiaji kwa kiasi kikubwa wanatatizika na kasi ndogo na huduma chache za 2G.[32]

Kuzimwa kwa intaneti kwa miaka mingi huko Tigray na jumuiya jirani zilizoathiriwa kunatoa picha wazi ya jinsi vitendo hivi vya ukatizaji vinaweza kuwa vya kuumiza na hatari. Kando na athari za harakati za kukatiza watu milioni sita wa eneo hilo kutoka sehemu nyingine za dunia, kukatika kwa mawasiliano kunakoendelea kumesababisha vitisho vingi kwa haki za kimsingi za wana-Tigray.[33] Kwa kuwa ni mojawapo ya njia ndefu zaidi za kuzimwa kwa intaneti bila kusitishwa kuwahi kutokea wakati wa mzozo unaoendelea, pia imekuwa na athari mbaya kwa maisha ya watu.[34] Kufungiwa huko kulitoa kifuniko kwa pande zinazopigana kufanya uhalifu ikiwa ni pamoja na mauaji ya kimfumo na yaliyoenea, ubakaji na unyanyasaji wa kijinsia dhidi ya vikundi vilivyo hatarini.[35] Pia ilizuia utoaji wa misaada ya kibinadamu kwa jamii zilizoathirika zinazokabiliwa na njaa na uhaba mwingine. Hakuna mtu angeweza kutegemea huduma za kimsingi kama vile afya, benki, ajira, na elimu.

### Kisa kuhusu athari ya kuzima mtandao: Tigray

**"Nakumbuka siku ambazo niliamka na kujaribu kupiga nambari tofauti kila siku nikitumaini kwamba mmoja wa wanafamilia wangu ataweza kupokea. Ni hali mbaya zaidi ambayo mwanadamu anaweza kuwa ndani, [bila kujua] ikiwa wanafamilia wako wako hai au la. Kusikia [ripoti] mashambulio yote ya ndege zisizo na rubani kwa raia zilizotumika kulinifanya nipoteze akili. Sikuweza kuzingatia shule na kazi yangu. Nilikuwa nikiwaona ndugu zangu kwenye ndoto na nilitaka kuongea nao lakini sikuweza kwa miaka 2+. Hata sasa bado sijaweza kuwasiliana na wanafamilia wachache kwa sababu ufikiaji wa mtandao haurudishwi katika miji yote ya mkoa wa Tigray."**

Mwanamke mchanga wa Kitigray anayeishi U.S

Licha ya mzozo wa wenyewe kwa wenyewe na kuzimwa kwa mtandao Tigray kuwa wa kutisha, wanaharakati wa haki za kidijitali na watetezi wa haki za binadamu walionyesha uthabiti mkubwa, wakiendelea kuvuta

---

**28** Access Now (2022). *ECOWAS Court victory: Twitter ban in Nigeria declared unlawful*. Retrieved February 17, 2023, from https://www.accessnow.org/ecowas-court-nigeria-unlawful-twitter-ban/.

**29** Monitor (2022). *Facebook to remain shut as govt talks with tech giant stall*. Retrieved February 22, 2023, from https://www.monitor.co.ug/uganda/news/national/facebook-to-remain-shut-as-govt-talks-with-tech-giant-stall-3912172/.

**30** Access Now (2023). *After years in the dark, Tigray is slowly coming back online*. Retrieved February 17, 2023, from https://www.accessnow.org/tigray-shutdown-slowly-coming-back-online/.

**31** United Nations News (2022). *Ethiopia: Peace agreement between Government and Tigray 'a critical first step': Guterres*. Retrieved February 17, 2023, from https://news.un.org/en/story/2022/11/1130137/.

**32** *See supra* note 30.

**33** Access Now (2022). *Stranded, suffocated, and in pain: 15 stories from Tigray's internet siege*. Retrieved February 17, 2023, from https://www.accessnow.org/15-stories-from-tigrays-internet-siege/.

**34** Tghat (2022). *Impact of the Internet Shutdown in Tigray*. Retrieved February 17, 2023, from https://www.tghat.com/2022/02/24/impact-of-the-internet-shutdown-in-tigray/.

**35** Global Voices (2021). *Vicious mass rape of women has become a weapon against the Tigray in Ethiopian war*. Retrieved February 22, 2023, from https://globalvoices.org/2021/07/05/vicious-mass-rape-of-women-has-become-a-weapon-against-the-tigray-in-ethiopian-war/.

hisia za ulimwengu kwa ukiukaji wa haki unaofanyika katika jamii zao.[36] Kwa mshikamano, Access Now na muungano wa #KeepItOn zilifanya kazi na washirika wa ndani na wanachama wa diaspora ya Ethiopia ili kukuza sauti za wana-Tigray na kudai uwajibikaji kwa kuzima mtandao. Tulileta pamoja zaidi ya mashirika 100 ya mashirika ya kiraia na watu binafsi kutoka zaidi ya nchi 102 ili kuuhimiza Umoja wa Afrika kuchukua hatua kukomesha kufungwa kwa mtandao.[37] Wakati Ethiopia ilikuwa mwenyeji wa Kongamano la kila mwaka la Utawala wa Mtandao, yaani Internet Governance Forum, mnamo Novemba 2022, muungano wetu ulifanya kazi kuisogeza hali ya Tigray juu ya ajenda ya kimataifa.[38]

*** Tazama sura ya Mashariki ya Kati na Afrika Kaskazini (MENA) kwa maelezo kuhusu kuzimwa kwa huduma za mtandao nchini Algeria,Tunisia, Libya na Sudan.*

**36** Tghat (2022). *Open letter to the Internet Governance Forum*. Retrieved February 17, 2023, from https://www.tghat.com/2022/09/11/open-letter-to-the-internet-governance-forum/.

**37** Access Now (2022). *Petition: AU must take urgent steps to help reconnect Tigray to the internet*. Retrieved February 22, 2023, from https://www.accessnow.org/petition-au-reconnect-tigray/.

**38** Internet Governance Forum (2022). *Seventeenth Meeting of Internet Governance Forum*. Retrieved February 6, 2022, from https://mail.intgovforum.org/IGF2022_summaryreport_final.pdf/.

## JALADA LA NYUMA

Kampeni ya #KeepItOn inaunganisha na kupanga mashirika ya kimataifa kwa juhudi za kukomesha uzimaji wawa mtandao. Kampeni hiyo ilizinduliwa na muungano wa takriban mashirika 70 mwaka wa 2016 katika RightsCon huko Silicon Valley. Uanachama wa muungano huo umeongezeka kwa kasi hadi zaidi ya wanachama 300 kutoka nchi 105 duniani kote kuanzia mashirika ya kiraia, haki, na makundi ya utetezi hadi vituo vya utafiti, mitandao ya utambuzi, taasisi na mashirika ya vyombo vya habari.

Ripoti hii ni uchapishaji wa Access Now kwa muungano wa #KeepItOn na iliandikwa na Zach Rosson, Felicia Anthonio, na Carolyn Tackett kwa ushirikiano na timu ya Access Now.

Waandishi wangependa hasa kuwashukuru Sage Cheng, Donna Wentworth, Marwa Fatafta, Raman Jit Singh Chima, Wai Phyo Myint, Golda Benjamin, Anastasiya Zhyrmont, Natalia Krapiva, Ángela Alarcón, Bridget Andere, Ji Yeon Kim, Jaimee Kokonya, Namrata Maheshwari, Peter Micek, Kassem Mnejja, Laura O'Brien, Gaspar Pisanu, Agneris Sampieri, Dhevy Sivaprakasam, Chetna Kumar, Alexia Skok, na Megan Kathure, kwa michango yao. Wangependa kuwashukuru Data4Change, Software Freedom Law Center India (SFLC.in), Yodet, Digitally Right, Miaan Group, Cloudflare, Internet Outage Detection and Analysis (IODA), Myanmar Internet Project, Athan, Kentik, Open Observatory of Network Interference (OONI), na wanachama wengine wa muungano wa #KeepItOn kwa kutoa taarifa muhimu na maarifa kuhusu uchunguzi wa matukio, kukagua data na vyanzo, na kuchangia ripoti. Hitilafu zozote, uwakilishi mbaya, au usahihi ni wetu

Ubunifu na taswira ya data umefanywa na Sage Cheng.

## Ujumbe juu ya data yetu

Ripoti hii ya #KeepItOn inaangazia matukio ya kuzima kwa intaneti yaliyothibitishwa na Fikia Sasa na muungano wa #KeepItOn mwaka wa 2022. Ingawa tunajaribu kuunda hifadhidata ya kina, data yetu inategemea vipimo vya kiufundi na pia maelezo ya muktadha, kama vile ripoti za habari au akaunti za kibinafsi. Vikwazo vya mbinu yetu vinamaanisha kuwa kunaweza kuwa na visa vya kuzimwa kwa mtandao ambavyo havijaripotiwa, na nambari zinaweza kubadilika ikiwa na wakati habari mpya itapatikana baada ya kuchapishwa. Kwa kusoma zaidi, tafadhali tembelea https://accessnow.org/keepiton-data-methodology.

#KeepItOn

CC BY